**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

# KIGAMBONI 2022

## JARIDA LA ROBO YA PILI

Toleo Namba 2

Mwezi Oktoba - Disemba



Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan awasha mtambo (pampu) wa kutoa maji chini ya ardhi kwenye kisima kirefu (m 450) kwa ajili ya kuyapeleka kwenda kwenye tanki kubwa la maji lenye lita Milioni 15 lililopo Kigamboni.

Limeandaliwa Na:
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni

# YALIYOMO


> RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN AZINDUA MRADI WA MAJI KIGAMBONI

> NAIBU KATIBU MKUU OR-TAMISEMI AFANYA ZIARA MANISPAA YA KIGAMBONI,MPANGO UBORESHAJI MIUNDOMBINU SHULE ZA MSINGI WAPAMBA MOTO

> RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN ATOA ZAWADI ZA SIKUKUU ZA MWISHO WA MWAKA 2022 KATIKA KITUO CHA HISANI ORPHANAGE CENTER-KIGAMBONI

> UJENZI DARAJA SANGATINI WAANZA TSH. BILIONI 2.9 KUTUMIKA

> DC NYANGASA APIGA MARUFUKU MICHANGO HOLELA MASHULENI, AWAHIMIZA WAZAZI NA WALEZI KUHAKIKISHA WATOTO WANARIPOTI MASHULENI

> TSH. MILIONI 500,549,836.41 KUTOKA MAPATO YA NDANI KUTUMIKA KWA AJILI YA UKARABATI MIUNDO MBINU SHULE ZA SEKONDARI MANISPAA YA KIGAMBONI

> KUELEKEA SHEREHE ZA CHRISTMAS NA MWAKA MPYA MKUU WA WILAYA KIGAMBONI ATAKA AMANI, UTULIVU NA USALAMA,AONGEA NA WATENDAJI KATA

> KAMATI YA UFUATILIAJI MRADI WA MADARASA 10 YA KAPU LA MAMA MANISPAA YA KIGAMBONI WAFANYA TATHMINI YA UJENZI

> SERIKALI YAJIKITA KUHAKIKISHA INABORESHA ELIMU YA AWALI NA MSINGI, MAZINGIRA YA UJIFUNZAJI NA UFUNDISHAJI TANZANIA

> (MTAKUWA) WILAYA YA KIGAMBONI WAANDAA MKAKATI ULINZI MWANAMKE NA MTOTO

> AFISA UTUMISHI MKUU MANISPAA YA KIGAMBONI ATOA BARAKA KWA WACHEZAJI WA TIMU YA WATUMISHI ,AWATAKA KUDUMISHA NIDHAMU WAWAPO MASHINDANONI MOROGORO

> RC MAKALLA AMSHUKURU RAIS SAMIA KUTOA FEDHA UJENZI WA MADARASA 618

> MANISPAA YA KIGAMBONI KUWEKA ALAMA ZA KATAZO YA UENDELEZAJI KWENYE MAENEO YOTE HATARISHI

> MADIWANI MANISPAA YA KIGAMBONI WAFANYA ZIARA KUKAGUA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

> MADIWANI MANISPAA YA IRINGA WAVUTIWA NA ENEO LA VIBANDA VYA MACHINGA KIGAMBONI, IRINGA MC KUIGA MFANO HUO

> ZOEZI LA ARDHI CLINIC KIGAMBONI LAFANIKIWA ,HATI 190 ZATOLEWA PAPO HAPO,KAMISHNA MKOA APONGEZA

> KAPU LA MAMA KIGAMBONI WANUFAIKA MADARASA 10 YAJENGWA

# RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN AZINDUA MRADI WA MAJI KIGAMBONI

Tarehe 11, Novemba, 2022

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali inakwenda kutekeleza ujenzi wa bwawa la maji la Kidunda mkoani Morogoro litakalotumika kukusanya maji wakati wa mvua.

Rais Samia amesema hayo wakati akizundua miradi ya maji Kigamboni, kukabidhi mitambo ya kuchimba visima na ujenzi wa mabwawa pamoja na kukabidhi eneo la ardhi kwa mkandarasi wa mradi wa bwawa la maji la Kidunda.

Aidha, Rais Samia amesema bwawa hilo lenye thamani ya shilingi bilioni 329 litakalojengwa kwa kutumia fedha za ndani litawezesha kuwepo uhakika wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima jijini Dar es Salaam na maeneo ya mkoa wa Pwani ambayo kwa sasa yanategemea maji ya Mto Ruvu.

Ujenzi wa bwawa hilo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu 2022 mpaka 2025 ambapo utakapokamilika utachochea kasi ya maendeleo ya viwanda katika mkoa wa Pwani pamoja na Dar es Salaam.



Kwa upande mwingine, mradi wa maji wa Kigamboni utaimarisha huduma ya maji katika maeneo ya Temeke, Ilala na Kinondoni hivyo kupunguza ukali wa mgao wa maji.

Hali kadhalika, Rais Samia ameiagiza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuhakikisha inasambaza maji kwa wananchi katika wilaya ya Kigamboni kwa asilimia 100.

Rais Samia ameitaka Wizara ya Maji kutoa elimu kwa wananchi kuacha kuchoma misitu ovyo, kuchepua maji pamoja na kuingiza mifugo hasa wananchi wanaoishi kando ya vyanzo vya maji kwani vitendo hivyo husababisha upungufu wa maji.

MWISHO.

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN AKIZINDUA MRADI WA MAJI KIGAMBONI.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Maji Jumaa Aweso wakivuta kitambaa kuashiria uzinduzi wa Mradi wa maji Kigamboni ambao unatoa maji lita milioni 70 kwa siku kwa ajili ya wakazi wa maeneo mbalimbali Jijini Dar es Salaam tarehe 11 Novemba, 2022.**



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akibonyeza kitufe kuwasha mtambo (pampu) wa kutoa maji chini ya ardhi kwenye kisima kirefu (m 450) kwa ajili ya kuyapeleka kwenda kwenye tanki kubwa la maji katika eneo la Kigamboni Jijini Dar es Salaam tarehe 11 Novemba.**



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiangalia maji baada ya kuwasha mtambo (pampu) wa kutoa maji chini ya ardhi kwenye kisima kirefu (m 450) kwa ajili ya kuyapeleka kwenda kwenye tanki kubwa la maji katika eneo la Kigamboni Jijini Dar es Salaam tarehe 11 Novemba, 2022.**

# NAIBU KATIBU MKUU OR-TAMISEMI AFANYA ZIARA MANISPAA YA KIGAMBONI,MPANGO UBORESHAJI MIUNDOMBINU SHULE ZA MSINGI WAPAMBA MOTO

Tarehe 16 Novemba, 2022

Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI ndg.Ramadhani Kailima amefanya ziara katika Manispaa ya Kigamboni kwa nia ya kukagua miradi pamoja na kutembelea shule za msingi zenye changamoto za miundo mbinu.

Akiwa katika ziara hii Ndg.Kailima amepitia shule takribani tano na kufanya ukaguzi wa miundo mbinu inayohitaji ukarabati na mapungufu upande wa madawati,matundu ya vyoo,ofisi za walimu.Shule zilizotembelewa ni AboudJumbe,Kidete,Kibugumo, Mjimwema na Kisota.

Aidha katika ziara hiyo ndg.Kailima amejionea uchakavu wa madarasa mbalimbali yanayohitaji kukarabatiwa,upungufu matundu ya vyoo,upungufu wa madawati na madarasa na kujazana kwa wanafunzi katika madarasa kutokana na kutotosheleza.

Akizungumza amesema mapungufu yote aliyoyashuhudia ameyachukua kwa ajili ya kwenda kuyawasilisha ili yafanyiwe kazi kupitia Mpango huu wa serikali ya awamu ya sita ambapo sasa inaenda kuboresha miundo mbinu ya shule za msingi kama ilivyofanya kwa shule za sekondari.



***"Tunamshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuja na mpango huu ambao sasa unaenda kutatua changamoto kwa upande wa shule za Msingi."***

Alisema Naibu Katibu Mkuu OR - TAMISEMI Ndg. Ramadhani Kailima

Pamoja na ukaguzi wa miundo mbinu Naibu Katibu Mkuu amekagua pia baadhi ya madarasa ya kidato cha kwanza yanayojengwa hivi sasa kupitia fedha za kapu la mama ambapo kwa Manispaa ya Kigamboni ilipata shs.Mil.200 kutekeleza ujenzi wa madarasa 10.

Pamoja na hayo amegusia suala la udhalilishaji wa watoto kushika kasi hivyo amewataka walimu kuwa karibu na wanafunzi ili kuyajua wanayopitia kwa upande huo na ameshauri kuwepo kwa Dawati linaloshughulika na maswala ya udhalilishaji wa wanafunzi.Pia suala la madawa ya kulevya halikuwa nyuma kwani amewataka walimu kuwa makini na wauzaji wa biskuti na pipi wanaofika mashuleni kuuzia watoto kwani umezuka mtindo wa kuweka madawa ya kulevya katika pipi na biskuti jambo linalopelekea watoto kujiingiza katika madawa ya kulevya bila kujijua.

Ziara hii ni kufuatia mpango huo wa uboreshaji wa miundombinu kwa shule za msingi ambao serikali ya awamu ya sita ya Mh.Samia Suluhu Hassan imeamua kuutekeleza ili kuboresha miundo mbinu ya shule za msingi,hivyo unafanyika ukaguzi katika mashule kubaini maeneo yote yanayohitaji kuboreshwa, aidha ni utekelezaji wa Ilani ya chama cha Mapinduzi katika kuwaletea wananchi maendeleo.

MWISHO.



***"Nawaomba mfuatilie wanafunzi kwa ukaribu ili kubaini unyanyasaji wa kijinsia unaendelea katika Jamii na Familia zao kwani kuna matukio mengi yanaendelea ya udhalilishaji katika jamii zetu, walimu mna nafasi kubwa ya kuisaidia Serikali kuyabaini hayo na kuripoti kwa ajili ya kuwachukulia hatua wahusika"***

Alisema Naibu Katibu Mkuu OR - TAMISEMI Ndg. Ramadhani Kailima

# RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN ATOA ZAWADI ZA SIKUKUU ZA MWISHO WA MWAKA 2022 KATIKA KITUO CHA HISANI ORPHANAGE CENTER-KIGAMBONI

**-Waziri Dkt. Dorothy Gwagima (Mb) akabidhi zawadi hizo kuashiria Uzinduzi rasmi wa Utoaji wa zawadi hizo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.**

**-Watoto wenye Uhitaji katika kituo cha Hisani Orphanage Center wamshukuru Mhe Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Dkt. Dorothy Gwagima amekabidhi zawadi za sikukuu za mwisho wa mwaka zilizotolewa na Rais Mhe. Dkt Samia Suluhu katika kituo cha Kulelea watoto wenye mahitaji maalum kinachoitwa Hisani Orphanage Center Kigamboni-Dar es Salaam.

Mhe Dkt Dorothy Gwagima amekabidhi zawadi mbalimbali katika kituo hicho ikiwemo Mchele, Juice, Mafuta ya kupikia, Maharage, Chunvi na Mbuzi wawili (2)

Akikabidhi Zawadi hizo Mhe Dkt. Dorothy Gwagima amesema Rais Samia anawapenda sana ametoa zawadi hizo ikiwa ni salamu maalum kutoka kwake kwa niaba ya vituo takribani 29 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.




Utoaji wa zawadi hizo katika kituo hicho ni Uzinduzi rasmi ambapo kuanzia tarehe 22-24 Disemba wakuu wa Mikoa kwa kushirikiana na wadau wengine watakao guswa na watu wenye uhitaji wataendelea kutoa zawadi hizo katika maeneo yao au Mikoa yao.

Aidha Waziri amefurahishwa na namna kituo hicho kinavyotoa malezi bora ambapo kwa sasa kituo kinalea watoto zaidi ya 60.




***"Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatoa wito na hamasa kwa watanzania wote wenye upendo kote nchini kuungana naye kuendelea kuwakumbuka wenye uhitaji tunapoadhimisha Sikukuu za mwisho wa mwaka 2022 na mwaka mpya 2023 na anawatakia heri ya Sikukuu nyoote"***

Alisema Waziri wa Maendeleo ya Jamii Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)

Hata hivyo watoto wenye uhitaji katika kituo hicho wamshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Upendo wake kwao na wanamuombea kwa mwenyezi Mungu maisha marefu ili aendelee kuwatumikia.

Ifahamike kuwa hivi sasa nchini Tanzania kuna jumla ya Watoto 9011 ( Me 4897 na KE 4114 ) wanaopata huduma za msingi katika makao ya Watoto 325 yaliyosajiliwa yakiwemo 2 ya Serikali aidha  Jumla ya Wazee Wasiojiweza ni 263 ( Me 159 na KE 104 ) wanaohudumiwa Kwenye makazi 14 ya Serikali na wengine 537 ( Me 278 na KE 259 ) kwenye makazi ya watu binafsi.

MWISHO.

# UJENZI DARAJA SANGATINI WAANZA TSH. BILIONI 2.9 KUTUMIKA

Disemba, 2022

Serikali kupitia wakala wa barabara - TANROADS Dar es salaam imeanza ujenzi wa daraja muhimu la  Sangatini linalounganisha wilaya za Kigamboni na Mkuranga jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almas Nyangasa amesema kiasi cha shilingi bilioni 2.9 zitatumika kufanikish ujenzi wa daraja hilo,  mradi ambao utachukua muda wa miezi 12 kukamilika kwa mujibu wa mkataba na mkandarasi NGENDA Constructions .Co Ltd.

DC Nyangasa amesema hayo alipotembelea eneo la mradi na kusema Kuanza kwa ujenzi wa daraja hilo ni hatua kubwa katika kuboresha miundombinu inayosaidia kuunganisha wilaya hizo mbili.





***"Mhe. Rais Dkt. Samia anatupatia fedha zaidi kwenye kuboresha miundombinu, kukamilika kwa daraja hili kutasaidia sana wananchi kwa shughuli za kiuchumi na upatikanaji wa huduma kwa kuzingatia kuwa wakazi wengi wa upande wa Mkuranga wanapata huduma za kijamii kama hosp hapa Pemba Mnazi"***

Alisema Mkuu wa Wilaya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangasa

Mpaka sasa maandalizi ya eneo la kazi, vifaa , barabara za mwingiliano na ujenzi wa nguzo msingi vimefanyika.

Ujenzi wa daraja hilo umeanza Oktoba 3 mwaka jana na mkandarasi anatakiwa kuukabidhi ifikapo  Oktoba 2, 2023.

MWISHO.

# DC NYANGASA APIGA MARUFUKU MICHANGO HOLELA MASHULENI, AWAHIMIZA WAZAZI NA WALEZI KUHAKIKISHA WATOTO WANARIPOTI MASHULENI

Disemba, 2022

Mkuu wa wilaya ya Kigamboni Fatma Almas Nyangasa amewatahadharisha walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari kutoruhusu michango holela na isiyo na tija kwani mkakati wa serikali ni utoaji wa elimu bure ili kuwezesha watoto wengi kupata elimu ikiwa ni haki yao ya msingi.

DC Nyangasa amesema hayo leo hii alipopita kwenye shule mbalimbali za msingi na sekondari kukagua ni kwa kiasi gani watoto wameripoti shuleni na iwapo kulikuwa na changamoto katika siku hii ya kwanza yavkufungua shule katika mwaka 2023.

***“Mhe Rais Dkt. Samia ameelekeza fedha nyingi kwenye kuboresha miundombinu ya elimu Kigamboni, hivi karibuni tumepata shilingi milioni 200 kupitia kapu la mama tumejenga madarasa 10 mapya na viti ndani, yote hii ni kuwezesha watoto wetu wapate elimu bure”***

Alisema Mkuu wa Wilaya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangasa

Aidha, DC Nyangasa amewataka wazazi na walezi wenye watoto wanaotakiwa kuwa shule wanaripoti shuleni haraka, vinginevyo mzazi ama mlezi atawajibika kama hakutakuwa na sababu za msingi.



**Pichani DC Nyangasa alipotembelea shule mbalimbali za Msingi na Sekondari kujionea upokeaji wa Wanafunzi.**

Jumla ya watoto 4863 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza Kigamboni ambapo leo siku ya kwanza kufungua shule Wanafunzi 2586 Sawa na asilimia 53.1 wameripoti.





Kwa upande wa darasa la kwanza maoteo yalikuwa kuandikisha watoto 6981 na walioripoti ni 5400 sawa na asilimia 77 huku shule ya awali maoteo yalikuwa watoto 4291 na walioripoti ni 2742 sawa na asilimia 64.

MWISHO.

# TSH. MILIONI 500,549,836.41 KUTOKA MAPATO YA NDANI KUTUMIKA KWA AJILI YA UKARABATI MIUNDO MBINU SHULE ZA SEKONDARI MANISPAA YA KIGAMBONI

Disemba, 2022

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni katika Kipindi cha mwezi disemba 2022 imetoa kiasi cha shilingi.Mil.500,549,836.41 kwa ajili ya ukarabati wa miundo mbinu katika Shule za sekondari za Manispaa hiyo.

Miundombinu hiyo itakayokarabatiwa ni ukamilishaji wa maabara 1 zilizopo katika Kata ya Kisarawe II itakayogharimu mil.40,pia ukarabati wa jengo moja la utawala katika Kata hiyo ya Kisarawe II ambapo jengo hilo litagharimu shilingi mil.10 aidha ukarabati wa madarasa 4 yatakayotumia shilingi mil.8.

Kwa kata ya Mjimwema kiasi cha pesa mil.16 zitatumika kufanya ukarabati madarasa 8 yaliyopo katika Shule ya Kidete na Aboud jumbe,aidha katika Shule hiyo unafanyika ukarabati wa nyumba ya Mwalimu itakayogharimu mil.10 na Kisota ukarabati wa nyumba ya Mwalimu itakayogharimu mil.5,660,000, kidete umaliziaji wa bweni unagharimu mil.60 na kwa upande wa kisota matundu ya vyoo 5 yanatumia mil.3,kwa Kibugumo sekondari hapohapo Mjimwema itatumika mil.3 ujenzi wa matundu ya vyoo 5.






Kwa upande wa Kata ya Kibada madarasa 4 katika Shule ya Kibada na ujenzi wa matundu ya vyoo 10(5 katika Shule ya Kibada na matundu 5 shule ya Mizimbini)Jumla zinatumika mil. 21,889,836.90.

Ukamilishaji wa jengo la utawala 1,ukamilishaji madarasa 4 ,umaliziaji matundu 5 ya vyoo katika Shule ya Nguva pamoja na katika Shule ya Somangira Jumla itatumika mil.22 hayo yote ni katika Kata ya Somangira.

Katika Kata ya Kigamboni umaliziaji wa miundombinu shule ya sekondari Paul Makonda inatumika mil.255.

Kata ya pembamnazi yatakarabatiwa madarasa 4 na ukarabati wa  jengo la utawala Jumla ya mil.16 zinaenda kukamilisha kazi hiyo.





Kata ya Vijibweni Mil.16 zinaenda kukarabati madarasa 8,ambapo 4 shule ya Vijibweni na 4 shule ya Minazini .

Katika Kata ya Tungi madarasa 4 yatafanyiwa ukarabati ambapo Jumla ya shilingi milioni 8 zitatumika kukarabati madarasa hayo

**Pongezi kwa Mkurugenzi na Menejimenti ya Manispaa ya Kigamboni  kwa kuwezesha kupatikana kwa fedha Kutoka Mapato ya ndani  ili kuwezesha mazingira Bora ya kujifunza na kufundishia.**

**Ilani ya CCM inatekelezwa kwa vitendo.**

**KAZI IENDELEE.**

**MWISHO.**

# KUELEKEA SHEREHE ZA CHRISTMAS NA MWAKA MPYA MKUU WA WILAYA KIGAMBONI ATAKA AMANI, UTULIVU NA USALAMA,AONGEA NA WATENDAJI KATA

Tarehe 22 Disemba, 2022

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Almas Nyangasa amekutana na Kamati ya Ulinzi na usalama, Wenyeviti wa kata, Watendaji wa Kata na watendaji wa Mitaa lengo likiwa kuwataka kuhakikisha Amani na usalama nyakati za sikukuu za Christmas na mwaka mpya vinadumishwa.

Akiongea katika mkutano huo Mhe. fatma amewataka Watendaji hao kukaa na Kamati zao za usalama ngazi ya Kata na Mitaa na kuhakikisha hali ya usalama .

DC Nyangasa amesema hali ya usalama Kigamboni ni shwari lakini ni Muhimu kuendelea kujiimarisha na kuwa waangalifu huku akiwataka Wazazi na walezi kuhakikisha watoto wana uangalizi wa kutosha .

Utoaji wa taarifa mapema ni Jambo ambalo amelisisitiza pale ambapo wataona kuna jambo linatatiza ili liweze kufatiliwa na kushughulikiwa kwa wakati.



Aidha amewataka viongozi hao wa Ngazi ya kata na mitaa kuwajibika katika nafasi zao sambamba na kuwaelimisha wananchi katika Kata zao juu ya kufuata taratibu na kusherehekea sikukuu hizi kwa utulivu .

Katika suala la usafi amewataka kuendelea kusimamia kwa karibu na kuhakikisha mazingira safi bila kusahau kuwahimiza wananchi kusafisha maeneo yao.



Akizungumza OCD wa Wilaya ya Kigamboni mara baada ya kukaribishwa na Mkuu wa Wilaya ndugu Tobias Walelo Amemuhakikishia Mh.Fatma Nyangasa kuwa jeshi la polisi Wilaya ya Kigamboni limejipanga vizuri kuwalinda wananchi na Mali zao.

OCD Walelo ametumia mkutano huo kutahadharisha mikusanyiko isiyo ya lazima na wale wanaoenda kuogelea beach kuwa waangalifu .

Aidha,OCD Walelo amewataka Watendaji kuhakikisha viashiria vyovyote vya uvunjifu wa Amani viripotiwe haraka.

MWISHO.



**Sehemu ya Viongozi mbalimbali wakiwemo Watendaji wa Kata na Mitaa wakiwa ndani ya Kikao cha kamati ya Ulinzi na Usalama kilichoingozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangasa.**

# KAMATI YA UFUATILIAJI MRADI WA MADARASA 10 YA KAPU LA MAMA MANISPAA YA KIGAMBONI WAFANYA TATHMINI YA UJENZI

Tarehe 23/12/2022.

katika ukumbi wa Manispaa ya Kigamboni chini ya Mwenyekiti wa kamati Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni ndg.Erasto Kiwale wamefanya tathmini ya ujenzi wa madarasa 10 ya KAPU LA MAMA.

Akizungumza katika kikao hicho ndg.Kiwale amesema lengo la kikao hicho ni kukaa kwa pamoja kufanya tathmini ili kwa pamoja kujua kila hatua iliyofikiwa na kubaini kama kuna maboresho yoyote yanayohitajika kuelekea kwenye tukio la makabidhiano hivi karibuni.

Akizungumza ndg.kiwale amemshukuru Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha kupatikana kwa madarasa hayo kumi ambayo yanaenda kutatua tatizo la msongamano kwa wanafunzi lakini pia ameishukuru Kamati kwa kusimamia utekelezaji wa ujenzi na ushirikiano waliouonyesha tangu mwanzo na sasa maradi umekamilika,aidha amewataka kutoa ushirikiano na kuwa na Kasi hiyohiyo katika miradi mingine inayoendelea na itakayokuja.

Nao wakuu wa shule ambao walikuwa ndio wasimamizi wa karibu katika kutekeleza wametoa taarifa za ujenzi kwa kila darasa katika shule mbalimbali ambapo taarifa hiyo imeonyesha hatua zipo mwishoni na ujenzi umekamikika kwa asilimia 100.



Katika kuzungumzia uzoefu walioupata katika mradi huu ndg. kiwale amesema ana Imani kila mmoja amepata uzoefu mkubwa katika nyanja mbalimbali kwenye utekelezaji wa mradi huu ikiwepo gharama za vifaa, gharama za mafundi,ujenzi wa madarasa bora,namna ya kudhibiti ili kupunguza gharama nakadharika ambapo amesema na kwa miradi mingine tathmini za namna hii zitaendelea kufanyika.

Wakiongea walimu wakuu mara baada ya kupewa fursa wamesema wanashauri serikali kuangalia upya na kufanya tathmini juu ya gharama kamili za ujenzi wa darasa kwani gharama zinatofautiana sana kutoka eneo moja mpaka jingine .

Akimalizia wakati akifungua kikao ndg.Kiwale amewataka kuhakikisha mazingira ya nje na ndani ya madarasa hayo kuwekwa katika hali ya usafi na mazingira ya shule zao kwa ujumla.

Manispaa ya Kigamboni katika mradi wa KAPU LA MAMA ilinufaika kwa kupata shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 10.

# SERIKALI YAJIKITA KUHAKIKISHA INABORESHA ELIMU YA AWALI NA MSINGI, MAZINGIRA YA UJIFUNZAJI NA UFUNDISHAJI TANZANIA

Disemba, 2022

Jumla ya vyumba vya madarasa 12000 vya shule za awali na msingi za serikali hapa nchini vinatarajiwa kujengwa kwa kipindi cha miaka mitano kupitia mradi wa BOOST katika maeneo yenye upungufu au msongamano wa wanafunzi.

Hayo yamebainika katika mafunzo ya siku mbili ya utekelezaji wa mradi huo kwa wajumbe wa timu za utekelezaji za mikoa na Halmashauri kutoka mikoa ya Dar es salaam, Dodoma,Pwani Morogoro na Bagamoyo .Tshs Trillion 1.15 zinatarajiwa kutumika kutekeleza mradi huu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia.

Pamoja na madarasa hayo 12000 kujengwa pia vifaa vya tehama kwa shule za msingi vitanunuliwa aidha uwezeshwaji wa vituo vya mafunzo kwa walimu 8000 utatekelezwa pamoja na mpango wa shule salama 6000 utatekelezwa na kuongeza uandikishwaji wa elimu ya awali kufikia asilimia 85 .

Utekelezaji wa mradi huu utakuwa wa lipa kwa matokeo,hivyo timu za utekelezaji zitapaswa kufanya kazi kwa matokeo ili kuwezesha mradi kuendelea na kusaidia kuondosha changamoto zilizopo katika elimu ya awali na msingi.



Malengo ya program ni kuboresha upatikanaji fursa Sawa katika ujifunzaji Bora wa elimu ya awali na msingi Tanzania bara.boost ni sehemu ya Mpango wa lipa kulingana na matokeo katika elimu awamu ya pili (EPforR II) na unachangia utekelezaji wa Mpango wa maendeleo wa sekta ya Elimu wa miaka mitano 2021/22 na 2025/26.

Mradi huu utaboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji,ujuzi na ubora wa walimu katika kufundisha pamoja na kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za utoaji huduma za elimu ngazi za Halmashauri.

Mafunzo haya ya siku mbili kwa kanda ya mashariki yanamalizika Leo 17/12/2022 mkoani Morogoro.

# (MTAKUWA) WILAYA YA KIGAMBONI WAANDAA MKAKATI ULINZI MWANAMKE NA MTOTO

Disemba, 2022

Kamati ya ulinzi na usalama wa mwanamke na mtoto Wilaya ya Kigamboni leo Desemba 7, 2022 imeketi na kuweka maazimio wanayotarajia kuyatekeleza ifikapo january 2023 huku wakipanga kujipima ifikapo mwezi Machi 2023.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Afisa Ustawi kiongozi wa Manispaa ya Kigamboni Bi. Sereti Kiroya alisema kuwa kamati hiyo haina budi kuweka mpango mkakati na kuanza kuutekeleza mapema Januari 2023 huku wakiweka mapendekezo ya kujipima ifikapo machi 2023 kwenye vikao vya robo ya tatu.

***"Sisi kama kamati tumejiwekea mipango nane ambayo kimsingi inatupasa kuitumia kama sehemu ya majukumu yetu huku tukitumia mipango hiyo kama chombo cha kupima utendaji wetu wa ukamilifu wa yale tuliyojipangia,"***

Alisema Bi Kiroya

Aliitaja mipango waliyojiwekea kuwa ni pamoja na kukutana na kamati za ulinzi ngazi ya kata kwa lengo la kuwapa elimu watakayoitumia kufikisha kwa jamii, kuunda vikundi vya malezi kwenye maeneo ambayo havipo na kuvisimamia vile vilivyopo ili viweze kufanya kazi tarajiwa.



Naye Afisa Elimu vijana katika Manispaa hiyo Grace Muya alitoa pendekezo lake kwa kuitaka Kamati itoe elimu mashuleni hasa nyakati ambazo vikao vya wazazi na walimu vinafanyika kwani takwimu zinaonesha kuwa ukatili mkubwa wa kijinsia unaanzia ngazi ya familia.

KIkao hicho cha kamati ya ulinzi wa mwanamke na watoto kimehudhuriwa na wajumbe kutoka idara mbali mbali ikiwa na lengo la kuendeleza mpango mkakati wa Taifa wa kutokomeza ukatili wa wanawake na watoto (MTAKUWA).

MWISHO.

## AFISA UTUMISHI MKUU MANISPAA YA KIGAMBONI ATOA BARAKA KWA WACHEZAJI WA TIMU YA WATUMISHI ,AWATAKA KUDUMISHA NIDHAMU WAWAPO MASHINDANONI MOROGORO

Hayo yamejiri katika kikao cha pamoja kati ya wachezaji wa timu ya watumishi KGMC ya mpira wa miguu na mpira wa mikono wanaoenda mkoani Morogoro katika mashindano ya SHIMISEMITA.

Akizungumza mara baada ya Afisa Michezo wa Manispaa kuwatambulisha wachezaji hao watumishi wa timu ya mpira wa mikono na miguu Mkuu wa Idara usimamizi wa rasilimali watu na utawala Bi. Tabia Nzowa amesema Mashindano haya ya SHIMISEMITA ni utekelezaji wa maagizo ya Wizara ya Michezo na utamaduni ambapo wizara imetoa muongozo maalum katika kutekeleza agizo hili nasi Manispaa ya Kigamboni tumeitikia agizo hilo na kuhakikisha kwa kila hali tunalitekeleza.

Akiongelea kuhusu faida za Michezo Bi.Tabia amesema michezo ni Afya,lakini pia michezo hudumisha umoja baina ya wanajamii na si hivyo tu kupitia michezo inasaidia kukutanisha marafiki wapya na NI burudani inayosaidia hata kutoa mgandamizo wa akili na kuifanya akili itulie.

Aidha amesisitiza wakazingatie nidhamu watakapokuwa katika mashindano hayo wakumbuke kuwa wao ni watumishi wa umma hivyo hawana budi kulinda maadili na nidhamu ya kiutumishi wawapo katika mashindano hayo,wasijisahau kupitiliza kutakakopelekea kuwatoa katika lengo lililowapeleka na kusababisha kuwapunguzia ufanisi katika mashindano.



Pamoja na hayo amewapongeza kwa maandalizi ambayo wamekuwa wakiyafanya kwa ajili ya Mashindano haya mpaka sasa wamefikia katika hatua ya kwenda kushiriki mashindano.

***"Tunawapa baraka zote mkafanye vizuri mtuletee ushindi,naamini mtayazingatia yote mliyoelekeza na tuliyowashauri ,nae Mkurugenzi anawatakia kila la kheri na ushindi"***

Alisema Bi Tabia.



Timu hizo za mpira wa miguu na mikono wamejiandaa vyema kushiriki mashindano,aidha timu ya mpira wa miguu imefanikiwa kufikia ngazi ya Daraja la tatu na imesajiliwa.

MWISHO.

Kwa upande wake Afisa Michezo wa Manispaa Bi.Adolfina amemshukuru Mkurugenzi ndg.Erasto Kiwale na Menejimenti kwa kuhakikisha wanawawezeaha kushiriki mashindano haya ya SHIMISEMITA ,na kuahidi kuwa watajitahidi kwa kadri ya uwezo wao kuhakikisha wanarudi na ushindi.

Kwa upande wake Mratibu wa timu hiyo amemshukuru Mkurugenzi na Menejimenti kwa juhudi zao za kuhakikisha wanashiriki mashindano na ameahidi kuwa watarudi na ushindi.

# RC MAKALLA AMSHUKURU RAIS SAMIA KUTOA FEDHA UJENZI WA MADARASA 618

Oktoba 2022

- Asema Mkoa umepokea Bilioni 12 na milioni 360 kwa ajili ya Ujenzi huo.

- Aelekeza Ujenzi wa vyumba vya madarasa ufanyike kwa Force Account

- Ataka  Ujenzi kuzingatia Ubora, thamani ya pesa na kukamilika kwa wakati.

RC Makalla amesema hayo Oktoba 7,2022 katika kikao chake na Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari DSM, Ukumbi wa Arnatoglo Mnazimmoja, ambacho kilihudhuliwa na Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Maafisa Elimu, na Sekretarieti ya Mkoa ikiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa huo *Bi Rehema Madenge.

Mhe Makalla amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza Ilani ya CCM kwa vitendo kufuatia Mkoa huo kupewa kiasi cha Bilioni 12 na milioni 360 ambazo zimeelekezwa katika Ujenzi wa vyumba vya  madarasa 618 sawa na shule 108

Aidha RC Makalla ameelekeza kujenga Madarasa ya mfano kwa kutumia Force Account huku akisisitiza pesa hizo zikatumike kujenga madarasa na sio kulipa fidia.



Vilevile Mhe Makalla amewataka kusimamia vizuri zoezi hilo kwa kuzingatia thamani ya pesa na Ubora bila kusahau kazi ifanyike kwa wakati ifikapo Novemba 30,2022  Ujenzi uwe umekamilika.

Sambamba na hilo RC Makalla amesema amepokea migogoro 41shule za Sekondari na 25 Shule za msingi ya uvamizi wa Ardhi maeneo ya shule hivyo amewataka *Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kwenda kumaliza migogoro hiyo kwa kuyatembelea maeneo hayo, kuyakagua, Kuyajua vizuri maeneo hayo na kuweka mipaka.

RC Makalla ameelekeza migogoro yote ikashughulikiwe kwa ufanisi na apatiwe taarifa ya Utekelezaji wa zoezi hilo.

Kwa Upande wa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe Godwin Gondwe kwa niaba ya wakuu wa Wilaya wengine amemhakikishia Mkuu wa Mkoa kwenda kutekeleza maagizo yake aliyotoa ili ifikapo Januari 2023 wanafunzi waingie katika vyumba hivyo vya madarasa.

# MANISPAA YA KIGAMBONI KUWEKA ALAMA ZA KATAZO YA UENDELEZAJI KWENYE MAENEO YOTE HATARISHI

Tarehe 26/10/2022

Baraza la Madiwani limemuagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni pamoja na timu ya mejimenti kuweka alama za katazo ya uendelezaji kwenye maeneo yote hatarishi na kuandaa michoro pamoja na kuandika andiko litakalosaidia kutafuta ufadhili utakaosaidia kujenga mkondo maalumu wenye nguvu ya kukusanya maji kuelekea baharini ili kunusuru Makazi ya watu yanayoathirika na maji yanayotawanyika kutoka kwenye bwawa la Boko linalochukua maji kuoka maeneo mbalimbali kuelekeza baharini.

Akizungumza wakati wa Mkutano wa Baraza lililofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa Meya wa Kigamboni Mhe. Ernest Mafimbo amesema Mtaa wa Magogoni ni eneo ambalo linaathirika kwa asilimia kubwa kwani miundombinu ya kumwaga maji kutokea Daraja la Nyerere kueelekea baharini yanapita kwenye mkondo huo ambao unapita kwenye bwawa la boko lililopo kwenye mtaa huo hivyo ,kipindi cha mvua nyumba nyingi zinazungukwa na maji na kusababisha athari kwa watu na makazi kutokana na utambalale wa mkondo huo.

Akizungumzia upande wa udhibiti wa maambukizi ya virusi vya Ukimwi Meya amesema wamewaagiza wataalamu kurejesha utaratibu wa kupanga ratiba ya kuonesha sinema za uelimishaji juu ya ukimwi kuona athari na kupata tahadhari ya kujiepusha kwani janga hili bado lipo kwa kuangalia takwimu za kwenye vituo vyetu



Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Kimbiji Mhe. Sanya Bunaya amesema kuwa wananchi wamejishahu na kutumia njia ambazo sio sio sahihi za kujikiinga na maambukizi ya virusi vya ukimwi na kuacha kufuata maelekekezo ya wataalamu ya namna bora ya kujikinga na maambukizi hali inayopelekea ongezeko la maambukizi hayo.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kigamboni Mhe. Yahaya Shabani amesema anashukuru kushiriki kikao cha Baraza la Madiwani kwa mara ya kwanza tangu kuchaguliwa kwake, ameona kigamboni inaendelea kukua kwa kasi hivyo kwa kusikiliza hoja za wataalamu na Madiwani anaamini itaendelea kufunguka zaidi kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Ndg.Erasto Kiwale amesema amepokea maelekezo yote na atashirikiana na timu ya menejimenti ili kuhakikisha yanafanyiwa kazi kama yalivyoelekezwa kwa weredi.

Baraza la madiwani limejadlii pia taarifa za maendeleo za Kata na kamati zote.

# MADIWANI MANISPAA YA KIGAMBONI WAFANYA ZIARA KUKAGUA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Tarehe 19 Oktoba, 2022

Hayo yamejiri ambapo Madiwani wa Manispaa ya Kigamboni wamekagua miradi 3 kwa lengo la kujionea utekelezaji wake .

Miradi hiyo ni ujenzi wa Soko la mazao linalojengwa katika kata ya Somangila ambapo mpaka kukamilika kwake jumla ya Tshs.milioni 90 zitatumika.Wakiongea katika majumuisho wajumbe wamehitaji kujua mikakati iliyopo katika kulitangaza soko hilo kwa kuwa lipo hatua za mwisho ambapo kaimu mkurugenzi ndg.Lawiso alieleza kuwa kupitia maafisa maendeleo ya jamii walioko Kata na kitengo cha Mawasiliano Serikalini utangazaji utafanyika ili kuwafikia wananchi licha ya hilo pia vikao vya awali vilifanyika kwa ngazi ya Kata na wananchi na wafanya biashara kuwajulisha,lakini pia utafanyika mpango wa kuhamishia mnada ambao huwa unafanyika Gezaulole kuhamia katika soko hilo jipya.

Litakapokamilika soko hili litaiongezea halmashauri mapato kupitia ushuru utakaokuwa unalipwa na wafanyabiashara watakaokuwa wanatumia soko hili, pamoja na kusogeza huduma Kwa wananchi wa eneo hili ambao hawana huduma ya Soko.





Mradi mwingine waliotembelea ni mradi wa uuzaji wa viwanja eneo la Uvumba Kata ya Kibada ambapo Manispaa imepima viwanja 355 kwa matumizi mbalimbali viwanja hivyo vinatarajiwa kuuzwa mapema hivi karibuni ambapo wamepata maelezo ya taratibu zilizobaki ili sasa kuanza zoezi rasmi la kuuza viwanja hivyo kwa wananchi,mradi huu unatarajiwa kuiongezea mapato Manispaa hii.

Pamoja na miradi hiyo MADIWANI pia wametembelea eneo la Manispaa la shamba la Amadori lenye ukubwa wa ekari 2717,ambapo moja ya ushauri uliotolewa ni kufanyike mikakati kulipima eneo hilo na kuanza kufanya mikakati ya kuhakikisha miundo mbinu inayotakiwa inafanyiwa mipango ya kuwekwa.

Ukamilikaji wa miradi hiyo itaongeza tija katika kuongeza mapato ya Manispaa,lakini pia kuongeza huduma bora Kwa wananchi ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Tawala CCM.Kazi iendelee.

MWISHO.

# MADIWANI MANISPAA YA IRINGA WAVUTIWA NA ENEO LA VIBANDA VYA MACHINGA KIGAMBONI, IRINGA MC KUIGA MFANO HUO

Novemba, 2022

Madiwani pamoja na watendaji wa Manispaa ya Iringa wamefanya Ziara katika Manispaa ya Kigamboni kwa lengo la kujifunza namna taratibu zote walizofuata hata kufanikisha ujenzi wa vibanda vya wamachinga na jinsi gani wanawapanga machinga lakini pia pamoja na ukusanyaji wa mapato katika Manispaa.

Akiongea mara baada ya Ziara ya kutembelea mradi wa ujenzi vibanda vya Machinga uliopo eneo la NAFCO, Soko jipya na la kisasa la Kibada,Soko la Dege na eneo la wafanyabiashara Ungindoni Meya wa Manispaa ya Iringa Mhe.Ibrahim Ngwada amesema wamenufaika Sana na Ziara hiyo wamejifunza Mambo ambayo hawakuyajua kabisa na kwa pamoja wataenda kutekeleza kama walivyojifunza hasa katika mradi wa ujenzi wa vibanda vya Machinga uliopo eneo la NAFCO

***"Sisi kama kamati , Kwa kweli eneo hili la ujenzi wa vibanda vya Machinga umetuvutia Sana na mara nasi tutaenda kutekeleza kama mlivyotufundisha na kutuelekeza,ni mradi shirikishi na unaoipunguzia Manispaa gharama lakini pia unaipatia mapato endelevu "***

Alisema Mhe. Ibrahim Ngwada

Aidha Madiwani hao walipata fursa ya kuuliza maswali mengi katika majumuisho na kupatiwa majibu sahihi kutoka kwa wataalam wa Manispaa.






Moja ya swali ilikuwa ni namna gani wamekuwa walichagua eneo la machinga ambapo walijibiwa kuwa Manispaa ilishirikisha wadau wote wakiwepo uongozi wa Machinga na ngazi zote kuanzia chini kwa wananchi jambo ambalo Madiwani hawa wa Iringa wametoa pongezi kwa Mahusiano mazuri na machinga kwani baadhi ya maeneo mengine Mahusiano na machinga imekuwa ni changamoto.

Huu ni mfululizo wa wageni ambao wamekuwa wakifika Manispaa ya Kigamboni kujifunza masuala mbalimbali hasa ya miradi inayoongeza mapato.Ikumbukwe Manispaa ya Kigamboni ilifanya vizuri katika mwaka wa fedha 2021/2022 hata kutambuliwa na kupongezwa.

# ZOEZI LA ARDHI CLINIC KIGAMBONI LAFANIKIWA ,HATI 190 ZATOLEWA PAPO HAPO,KAMISHNA MKOA APONGEZA

Tarehe 19/11/2022

Hayo yamejiri katika viwanja vya Mjimwema ambapo Manispaa ya Kigamboni kwa kushirikiana na Wizara ya ardhi na maendeleo ya Makazi iliweka Kituo cha muda (Ardhi clinic) kwa ajili ya ugawaji wa hati papohapo kwa wananchi,kutatua migogoro,kuwaelimisha wananchi kuhusiana na maswala mbalimbali yahusuyo ardhi ambapo Jumla ya hati 190
zimegawiwa kwa wananchi na Jumla ya migogoro 17 imetatuliwa.

Akizungumza Kamishna wa ardhi wa Mkoa wa Dar es salaam Idrisa Kayera amesema zoezi hili limetoa fursa kwa wananchi kuweza kuwakilisha migogoro yao na pia kupata hati zao kwa wakati huohuo,amesema Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo kwa Mh.Waziri wa ardhi na maendeleo ya Makazi Mh.Angelina Mabula kuhakikisha wananchi wanahudumiwa kuanzia ngazi ya Kata kwa ukaribu ambapo katika kutekeleza hilo sasa Makamishna wa ardhi wapo kila mkoa aidha na maafisa mipangomiji wapo pia lengo likiwa kutekeleza maelekezo ya Mh.Rais Samia Suluhu Hassan ya kutaka jitahada zifanyike kutatua changamoto za ardhi  na kuboresha huduma kwa wananchi.



Akiongelea suala la urasimishaji Kamishna Kayera amesema kwa kiasi kikubwa changamoto katika urasimishaji zimepungua ambapo changamoto iliyobaki ni upande wa wananchi kukamilisha malipo kwa wakati ili mambo yaende sawa kwa maana ya kukamilisha urasimishaji.Aidha ametoa taarifa juu ya maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mh.Angelina Mabula  juu ya kupungua kwa riba watakaolipia Kodi ya ardhi kabla ya tarehe 1/1/2023 hivyo wananchi wajitokeze kuwahi punguzo hilo mapema kabla ya muda kuisha. Bila kusita Kamishna Kayera ameipongeza Manispaa kwa kufanikisha zoezi la Kituo cha muda kushughulikia masuala ya ardhi kwa ufanisi mkubwa na wananchi kujitokeza kwa wingi katika zoezi hili.

***"kweli nawashukuru kwa kazi nzuri nimeona Kigamboni mnafanya kazi hongereni Sana "***

alisema Kamishna Kayera.

Nae Diwani wa  Kata ya Mjimwema Mh.Omary Ngurangwa amesema katika muda mfupi urasimishaji umeweza kutatua matatizo ya ardhi kwa kiasi kikubwa ambapo amesema katika Kata yake wameona matunda ya urasimishaji tofauti na changamoto ilivyokuwa mwanzoni hivyo wanaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa jinsi ilivyoshughulikia suala hili.

Nae Mkurugenzi wa Manispaa yae Kigamboni ndg.Erasto Kiwale akizungumza katika zoezi hilo amesema utekelezaji huu ni moja ya kutekeleza maagizo ya Mh.Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia ni utekeleza wa Ilani ya CCM katika kuboresha maisha ya wananchi ambapo kwa pamoja na Mkuu wa Wilaya Mh.Fatma Almas Nyangasa wamekuwa wakitekeleza kwa kusikiliza kero za migogoro ya ardhi na kuitatua. Aidha amewashukuru wadau walioshiriki pamoja nao katika kufanikisha zoezi hilo wakiwepo makampuni ya upimaji ardhi Property International na kampuni ya Tigo.Akiongelea kuhusu hati zilizotolewa mwishoni amesema hati 190 zimetolewa na migogoro 17 imepokelewa na kushughulikiwa,aidha anawataarifu wananchi kuwa zoezi litaendelea la kutoa hati katika ofisi za Manispaa hapo jumatatu hivyo wafike ofisini kuchukua hati zao na timu ya Wizara ya ardhi na maendeleo ya Makazi watakuwepo kuendelea na zoezi kwa kushirikiana na timu ya ardhi Kigamboni ,takriban hati  25 zitatolewa siku hiyo ya jumatatu.



**Sehemu ya Wananchi waliojitokeza na kupatiwa Hati zao papopapo.**

# MILIONI 438,111,518.39 KUNUFAISHA VIKUNDI 24 MIKOPO ASILIMIA 10 MANISPAA YA KIGAMBONI

Tarehe 17 Januari, 2023

Hayo yamebainika wakati wa mahojiano na Mratibu Dawati la uwezeshaji wananchi kiuchumi anashughulikia masuala ya mikopo kwa vikundi vya wajasiliamali katika Idara ya Maendeleo ya jamii Manispaa ya Kigamboni ndg.Masesa Mgonela Luanda ambapo amesema tayari vikundi 24 vilivyokidhi vigezo vimeshapitishiwa mikopo yao na taratibu zote zimefuatwa hivyo watapokea fedha zao ili kutekeleza yale waliyoyapanga kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za ujasiriamali na kujiinua kiuchumi.

Akichanganua jinsi mgawanyo wa fedha hizo ulivyo kulingana na makundi ndg. Masesa amesema katika fedha hizo shilingi 211,265,411.34 zitaenda kwa vikundi 11 vya wanawake,shilingi milioni 131,265,411.34 zitaenda kwa vikundi 7 vya vijana na shilingi milioni 95,580,695.71 zitaenda kwa vikundi 6 vya watu wenye ulemavu.



**Masesa Mgonela Luanda**
**MRATIBU DAWATI LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI MANISPAA YA KIGAMBONI**

Kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo ndugu Masesa anatoa wito kwa wanufaika wa mikopo hii kuwa fedha hizo sio zawadi inatakiwa kurejeshwa ili vikundi vingi zaidi viweze kunufaika kwani pesa zinavyorudi ndivyo zinavyosaidia kuwakopesha wengine na vikundi vingi vinapata kufaidika zaidi.

Mikopo hii ya asilimia kumi isiyo na riba hutolewa na kila halmashauri ambapo imewanufaisha na kuendelea kuwanufaisha makundi mbalimbali katika kujikwambua kiuchumi ikiwa ni dhamira thabiti ya serikali kuwakwamua wananchi kiuchumi na kuboresha maisha yao pamoja na kutekeleza Ilani ya CCM kivitendo.

# KAPU LA MAMA KIGAMBONI WANUFAIKA MADARASA 10 YAJENGWA

Katika kuboresha miundombinu ya elimu ya sekondari na kutatua changamoto za kukaa wanafunzi madarasani serikali imeendelea kutatua changamoto hizo kwa kuelekeza fedha katika sekta ya Elimu ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunza.



Manispaa ya Kigamboni ni moja ya Manispaa zilizonufaika na uboreswaji WA sekta ya Elimu ambapo katika mengi pia imepokea kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 10 yatakayotumika kwa wanafunzi wa kidato cha Kwanza kwa mwaka 2023.

Katika utekelezaji huo Manispaa imefanikisha kujenga vyumba hivyo kwa ustadi wa hali ya juu ambapo madarasa ni ya kisasa kabisa yenye vioo,feni na sakafu yenye marumaru.

Katika utekelezaji huo shule ya sekondari Kisota umepata darasa 1,Aboud jumbe darasa 1,Pembamnazi darasa 1, Kisarawe II darasa 1,Kibada darasa 1,Kidete darasa 1,Kimbiji darasa 1, Minazini darasa 1 na Mizimbini darasa 1.

Hongera serikali kwa kutekeleza Ilani ya CCM.

## SEHEMU YA VIPEPERUSHI VIKIONESHA UTENDAJI KAZI, UTOAJI ELIMU NA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI YA MAENDELEO















**Kalenda la Mwaka 2023 Lililochapishwa chini ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (KGMC ).**









Utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo unaendelea ndani ya Wilaya ya Kigamboni.






**LIMEANDALIWA NA;**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
KGMC

**Mwandishi;**

MARRY MAKOMBE

**Wahariri;**

JOSEPH SEMKIWA
HONORATA MBINDE

**Mpiga Picha;**

ADAM MWANDIKA

**Msanifu wa Jarida;**

ELIA PHAUSTINE